

HALMASHAURI YA WILAYA YA GEITA



(CIRCULAR RESOLUTION)

KUTOKA: KITENGO CHA USIMAMIZI WA MANUNUZI NA UGAVI

KWENDA: WAJUMBE BODI YA ZABUNI-HALMASHAURI YA WILAYA YA GEITA

TAREHE: 17/01/2022


YAH: OMBI LA KUENDELEA NA MCHAKATO WA UNUNUZI

Kwa mujibu wa Sheria ya Manunuzi namba 7 ya mwaka 2011 na Kanuni zake za mwaka 2013, kanuni ya 58, Bodi ya Zabuni imepewa mamlaka ya kutoa maamuzi bila kufanya kikao cha Bodi.

Kitengo cha Usimamizi wa Manunuzi na Ugavi kinawasilisha kwenu tangazo la kumpata local fundi wa kujenga wa jengo la dharura (Emergency Medical Department-EMD) na Wodi ya Watoto (Pediatric Ward) katika hospitali ya Katoro katika hospitali ya Katoro na jengo la Wagonjwa Mahututi (Intensive Care unit-ICU) katika hospitali ya Nzera zilizo ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Geita.

Kitengo cha Usimamizi wa Manunuzi na Ugavi kinaomba ridhaa ya Bodi ya Zabuni ili kuendelea na mchakato wa manunuzi kwa kutumia njia ya Force Account na pia matangazo yaliyoambatanishwa ili kumpata local fundis wa majengo tajwa.

Naomba kuwasilisha,


Joash F. Kunaga

**KATIBU BODI YA ZABUNI
HALMASHAURI YA WILAYA YA GEITA**

MAONI YA WAJUMBE


1. Ndugu: JANUARY BIKUBA

Nakubali/sikubali

Sahihi:

Tarehe:

MWENYEKITI



19/01/2022

2. Ndugu: SARAH N. YONA

Nakubali/sikubali

Sahihi:

Tarehe:

MJUMBE



25/01/2022


3. Ndugu: HELLEN E. MUGINI

Nakubali/sikubali

Sahihi:

Tarehe:

MJUMBE



25/01/2022

4. Ndugu: FARAJA KALUWA

Nakubali/sikubali

Sahihi:

Tarehe:

MJUMBE

.....

.....

5. Ndugu: RICHARD MWAKIHABA

Nakubali/sikubali

Sahihi:

Tarehe:

MJUMBE

.....

.....

HALMASHAURI YA WILAYA YA GEITA



TANGAZO LA KUTAFUTA LOCAL FUNDI UJENZI WA JENGO LA DHARURA (EMERGENCY MEDICAL DEPARTMENT EMD) KATIKA HOSPITALI YA KATORO

Halmashauri ya wilaya ya geita kwa kutumia force account inakaribisha maombi kwa mtu yeyote mwenye taaluma ya ujenzi wa jengo la dharura (Emergency Medical Department-EMD) katika hospitali ya Katoro iliyo ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Geita.

KAZI ZINAZOTAKIWA KUFANYIKA NI KAMA IFUATAVYO:

1. Kujenga msingi
2. Kumwaga jamvi
1. Kunyanyua kuta mpaka hatua ya gebo
2. Kupaua
3. Kuweka madirisha na milango
4. Kupiga plasta na sakafu
5. Kupaka rangi na kazi nyingine za ukamilishaji wa ujenzi
6. Kuweka vigae vya sakafu na ukuta na ceiling board
7. Kuweka mfumo wa umeme na kufunga vifaa vya umeme (ceiling fans, viyoyozi n.k.)
8. Kuweka mfumo wa maji na kufunga vifaa vya bomba

VIGEZO VINAVYOHITAJIKA

1. Barua ya maombi ya kazi ya ujenzi wa jengo la dharura (Emergency Medical Department-EMD) katika hospitali ya Katoro.

2. Cheti cha ufundi wa majengo kutoka chuo chochote kinachotambulika na serikali
3. Orodha ya kazi alizofanya ndani ya miaka mitatu iliyopita
4. Akaunti yake ya benki
5. Barua kutoka kwa mjumbe wa nyumba kumi/serikali ya mtaa
6. Awe anajua kusoma michoro ya majengo/wasifu wa kazi (Specifications)

MAELEZO YA JUMLA

1. Waombaji wote wawe watanzania
2. Waombaji waambatanishe maelezo binafsi (Cv) ikiwemo anuani na namba za simu ya mkononi
3. Waombaji waambatanishe nakala halisi za vyeti vya taaluma cheti cha kidato cha nne na cha kuzaliwa
4. Barua za maombi ziambatanishwe na picha Mbili 2 (passport size) zilizopigwa hivi karibuni
5. Mwombaji anapaswa kuwa na uwezo wa kusoma michoro, specification na BOQ pamoja na kuzifafanua kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu
6. Awe tayari kuendesha kazi na kupokea malipo baada ya kukaguliwa kazi na kuidhinishwa

JINSI YA KUTUMA MAOMBI

Barua zote za maombi ziandikwe kwa mkono zikiwa na jina kamili la muombaji pamoja na namba ya simu na zitumwe kwa anuani ifuatayo:

**KATIBU
BODI YA ZABUNI
HALMASHAURI YA WILAYA YA GEITA
S.L.P 139
GEITA**

TAREHE YA MWISHO KUPOKEA MAOMBI

Mwisho wa kupokea maombi ni siku ya Alhamisi tarehe 20/01/2022 saa 4:30 asubuhi. Na mara tu baada ya muda huo kutakuwa na zoezi la ufunguzi wa zabuni hiyo, hivyo muombaji au mwakilishi wake anatakiwa kuhudhuria katika ufunguzi.

John P. Wanga
**MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA YA GEITA**